

## TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)



### KUTHIBITISHA UDAHILI KWA WAOMBAJI WALIOCHAGULIWA NA CHUO ZAIDI YA KIMOJA.

Tume ya Vyuuo Vikuu Tanzania (TCU) inawatangazia waombaji wote wa udahili waliochaguliwa na chuo zaidi ya kimoja kuthibitisha udahili wao kwa kutumia namba maalum “confirmation code” iliyotumwa kupitia namba yake ya simu ambayo ilitumika wakati wa kufanya maombi ya udahili chuoni/vyuoni.

Waombaji wote wanaohusika na zoezi hili wanasisitizwa kuwa mwisho wa kuthibitisha udahili wao ni **Ijumaa tarehe 5/10/2018**. Waombaji hao wameganyika katika makundi mawili:

- 1) Waombaji waliodahiliwa na chuo zaidi ya kimoja katika awamu ya pili ([\*kuona majina yao bonyeza hapa\*](#)); na
- 2) Waombaji waliodahiliwa na chuo zaidi ya kimoja katika awamu ya kwanza ambao hadi sasa bado hawajajithibitisha katika chuo chochote ([\*kuona majina yao bonyeza hapa\*](#)).

Tume inapenda kuwatangazia Waombaji walio katika makundi haya kuwa wameshajulishwa kuhusu udahili wao kupitia ujumbe mfupi uliotumwa kwenye namba za simu za mikononi walizotumia wakati wa kuwasilisha maombi ya kujiunga na vyuo husika. Hivyo kila muombaji anatakiwa kufuata utaratibu ufuatao ili kujithibitisha:

- a) Kunakili namba maalumu (special code) iliyotumwa kwa njia ya ujumbe mfupi kwenye simu yake;

- b) Kuingia katika akaunti yake iliyo katika mfumo wa udahili wa chuo anachokipenda kati ya vile alivyochaguliwa; na
- c) Kuingiza namba hiyo maalumu katika mfumo wa udahili wa chuo anachokipenda ili kuthibitisha udahili wake katika chuo husika.

**Tume inapenda kuisisitiza kuwa, mwombaji anatakiwa kuthibitisha udahili wake ndani ya muda uliopangwa. Aidha, Tume inaviarifu vyuo vyote kuwa mifumo yao iwe wazi ili wale wanaotaka kuthibitisha udahili wao waweze kufanya hivyo. Waombaji pia wanakumbushwa kuwa matatizo yote yanahusiana na namba maalumu “codes” yari potuwe kwenye vyuo husika kwa utatuzi wa haraka zaidi.**

**Imetolewa na:**

**Katibu Mtendaji  
Tume ya Vyuo Vikuu  
Tanzania  
3/10/2018**